

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MKOJA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA MTWARA

Anuani ya Simu MTWARA

Simu Nambani 023-2333014

Fax Na: 023-2333194



OFISI YA MKUU WA MKOA

S.L.P. 544

MTWARA

Tarehe 30/07/2016

Taarifa kwa Umma

Jana Julai 29 Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Halima Dendego alikamilisha ziara yake ya siku Nne Wilayani Newala. Akiwa wilayani hapo Mhe. aliridhishwa na usimamizi mzuri wa shughuli za Maendeleo katika wilaya hiyo.

Moja ya mambo yaliyomfurahisha ni pamoja na jitihada kubwa inayofanywa na uongozi wa wilaya hiyo dhidi ya wananchi wanaovunja maadili na kurudisha nyuma maendeleo ya wilaya. Watu hao ni pamoja na wanaowapa ujauzito wanafunzi, Michezo inayovunja maadili maarufu kama vigodoro na 'Lete raha', Michezo ya 'Pool table' nyakati za kazi, usimamizi mzuri wa makusanyo ya fedha za ndani. Pia Ufuatiliaji na usimamizi imara kwa wakandarasi wanaopewa shughuli za ukandarasi katika wilaya hiyo.

Hata hivyo Mheshimiwa RC alisikitishwa na takwimu za maradhi ya saratani ya kizazi kwa akina mama ambapo asilimia 15 ya waliochunguzwa katika kipindi cha 2016/2017 waligundulika kuwa na maradhi hayo. Amemuagiza Mganga Mkuu wa Mkoa kuchukua hatua ili kubaini tatizo na hatimaye matibabu ya haraka.

Vilevile hakusita kuchukua hatua kwa baadhi ya maeneo ambayo hakuridhishwa na utendaji wake. Maeneo hayo ni pamoja na;

- Mkurugenzi asitishie mshahara wa watendaji wa Kata ambao wameshindwa kutekeleza agizo lake la benki ya matofali 1,000,000 ya kuchoma au 300,000 ya saruji kwa kila kijiji. Watendaji hao ni pamoja na yule wa kata ya Mdimba na Malatu.

- Timu ya ukaguzi ikaguwe gharama halisi za ujenzi Sekondari Mnyambe. Mheshimiwa RC hakuridhishwa na gharama za utengenezaji wa viti kwa shs 350,000 kwa kila kimoja.
- Wanafunzi 8 wa kijiji cha Mikumbi waliopata ujauzito na wenzi wao wakamatwe na kushtakiwa.
- Watendaji wote wa Serikali kata na vijiji wawe na ofisi iliyo na bendera ya Taifa.
- Uongozi Makukwe AMCOS uvunjwe. Uchaguzi mpya ufanyike. Viongozi hawa walibainika kula fedha za wananchi. Uchaguzi mpya ulipofanyika walichaguliwa tena wakati bado wanadaiwa kurudisha fedha walizokula. Pia aliwaagiza warudishe fedha hizo kabla ya Julai 29.
- Mheshimiwa RC aliahidi kuchangia jumla ya mifuko 500 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa mindombinu mbalimbali wilayani hapo. Mifuko 50 kwa ajili ya ujenzi Sekondari Mmulunga, 200 kwa ajili ya soko la kijiji cha Mtopwa, 100 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari Mpotola. 50 ujenzi wa kisima cha kuvunia maji Shule ya Msingi Makonga, 50 shule ya sekondari Kiuta, 100 zahanati ya Mcholi Godouni na 100 zahanati ya Mkulung'ulu.
- Pia aliahidi kutoa kompyuta 5 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Mpotola, 3 kwa ajili ya shule ya sekondari Makukwe.
- Vilevile Kikundi cha Tuhamasike cha ufugaji nyuki Mikumbi. Kipelekwe kwenye maonesho ya Nanenane. Pia atakipatia sh 1,000,000 ili kutunisha mfuko wa VICOBA.

Mhe. Mkuu wa Mkoa anawashukuru wananchi wote wa Wilaya ya Newala kwa ushirikiano wao waliouonesha kwa kipindi chote alichokuwa hapo. Aidha, ameahidi kutatua kero zote walizoziwasilisha kwake alipokutana nao na zile walizozituma kwa simu.

Imetolewa na;

Evaristy Masuha.

Afisa Habari. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mtwara.